

SHERIA YA NDOA NA TALAKA



WLAC

Kituo cha Msaada wa Sheria kwa Wanawake (WLAC)

S. L. P 79212, Dar es Salaam - Tanzania

Simu: +255 22 2664051

Nukushi: +255 22 2667222

Baruapepe: wlac@wlac.or.tz

Tovuti: www.wlac.or.tz

KIMETAYARISHWA NA:

Kituo cha Msaada wa Sheria kwa Wanawake (WLAC)

WAANDAAJI

Mary Njau
Alphonse Katemi
Athanasia Soka
Scholastica Jullu

MHARIRI

Winston Mosha

MICHORO

John John Simbe

©WLAC 2013

ISBN: 978 9987 733 04 0

YALIYOMO

1.0	Utangulizi	1
2.0	Maana ya ndoa	2
2.1	Hiari.....	2
2.2	Kudumu.....	2
2.3	Jinsi Tofauti.....	2
2.4	Maharimu	2
2.5	Umri	3
2.6	Kusiwe na ndoa inayoendelea	3
2.7	Kusiwe na Pingamizi	4
2.8	Mfungishaji ndoa awe na mamlaka	4
2.9	Kuwe na mashahidi	4
2.10	Wafunga ndoa wote wawepo	5
3.0	Aina za Ndoa	5
3.1	Ndoa ya mke mmoja	5
3.2	Ndoa ya wake wengi	5
4.0	Ufungishaji Ndoa	6
4.1	Kidini	6
4.2	Kiserikali	6
4.3	Kimila	6
5.0	Dhana ya Ndoa	6
6.0	Ndoa Batilifu	7
7.0	Haki za mwanamke katika ndoa	8
7.1	Usawa	8
7.2	Matunzo	8
7.3	Kumiliki mali	8
7.4	Kuishi katika nyumba ya ndoa	8
7.5	Kukopa	9
7.6	Uhuru wa kuishi popote	9
7.7	Kupata haki ya jasho lake	9
8.0	Kutengana na Talaka	10
8.1	Kutengana	10
8.2	Talaka	10



1.0 UTANGULIZI

Nchini Tanzania masuala ya ndoa yanaendeshwa na kusimamiwa kwa mujibu wa sheria za nchi. Sheria zinazosimamia masuala ya ndoa ni Sheria ya Ndoa, Sura ya 29 ya Sheria za Tanzania. Kitabu hiki kitazungumzia baadhi tu ya vifungu vya sheria hii. Sheria hii pamoja na mambo mengine inaeleza juu ya haki ya mke kumiliki mali katika ndoa na masuala ya mgawanyo wa mali endapo talaka itatolewa. Hali kadhalika kuongezeka kwa maambukizi ya virusi vya ukimwi katika jamii kumeleta changamoto kubwa kwa matumizi ya baadhi ya vifungu vya sheria hii na hasa vile vinavyoruhusu ndoa za wasichana wadogo walio chini ya umri wa miaka 18. Kitabu hiki kitawasaidia wanawake na jamii nzima ya Watanzania kupata ufahamu wa haki zao katika ndoa na kuzifuatilia.

2.0 MAANA YA NDOA

Kwa mujibu wa kifungu cha 9(1), cha Sheria ya Ndoa, sura ya 29 ya sheria za Tanzania, ndoa ni muungano wa hiari kati ya mwanaume na mwanamke unaokusudiwa kudumu kwa muda wa maisha yao yote.

Hata hivyo, muungano huo ili uweze kukamilika kisheria ni lazima mambo ya msingi yafuatayo yazingatiwe, nayo ni:

2.1 Hiari

Kifungu cha 16 kinaeleza kuwa muungano huo lazima uwe wa hiari. Udanganyifu au ulaghai, kurubuniwa kwa aina yoyote unafanya muungano usiwe wa hiari. Kama itathibitika kwamba hakukuwa na hiari basi muungano huo hauwezi kufikia hadhi ya kuwa ndoa. Watoto wa kike kuchaguliwa wanaume na wazazi/walezi wao au ndoa zinazoitwa za mkeka si ndoa kwa mujibu wa sheria hii ya ndoa.

2.2 Kudumu

Kifungu cha 9(1) kinabainisha kuwa muungano huo ni lazima uwe wa kudumu. Pia kifungu cha 12 kinazungumzia kuwa ndoa ni ya kudumu labda tu kama kuna kifo au talaka. Hivyo basi, kwa mujibu wa sheria hii, ndoa za mkataba wa muda fulani hazikubaliki.

2.3 Jinsi Tofauti

Muungano huo ni lazima uwe kati ya watu wa jinsi tofauti, yaani kati ya mwanamke na mwanaume kama kifungu cha 9(1) kinavyosema. Ndoa ya watu wa jinsi moja yaani mwanamke na mwanamke au mwanaume na mwanaume haina uhalali kisheria. Na mwanamke au mwanaume kisheria ni yule aliyezaliwa na viungo vya kike au vya kiume na sio aliyevipata baadaye.

2.4 Maharimu

Maharimu ni watu wenye undugu wa karibu wa damu ambao hawaruhusiwi kuoana. Kwa hiyo muungano huo usiwe wa watu

wenye undugu wa karibu ambao sheria imekataza watu wa uhusiano huo kuoana. Watu wenye uhusiano wa kindugu waliokatazwa kuoana wameelezwa katika kifungu cha 14. Kifungu hiki kinakataza mtu kuolewa/kumuoa dada, kaka, baba, mama, babu, bibi, shangazi, mjomba au mtoto aliyemuasili.

2.5 Umri

Kwa mujibu wa sheria hii ya ndoa ni lazima watu wanaotaka kufunga ndoa wawe wametimiza umri wa miaka 18 au zaidi. Hata hivyo sheria hii inaruhusu mwanamke kuolewa akiwa chini ya umri wa miaka 18. Kifungu cha 17 kinaeleza kwamba mwanamke ambaye hajatimiza miaka 18 anaweza kuolewa kwa idhini ya baba au kama baba amefariki basi mama na ikiwa wote wamefariki basi idhini hiyo yaweza kutolewa na mlezi wake.

Muhimu: Kuruhusu wasichana kuolewa chini ya umri wa miaka 18 kunawanyima fursa ya kuendelea na elimu na pia katika umri huo mdogo inawaweka katika mazingira magumu ya kuhimili majukumu ya ndoa, hivyo kuhatarisha afya yao kwa kutokuwa na elimu ya uzazi.

Pia kwa kuzingatia mazingira ya sasa ya UKIMWI wasichana hawa wadogo wanakuwa katika hatari zaidi ya kuambukizwa virusi vya UKIMWI kutokana na uelewa wao mdogo na pia kutokuwa na nafasi ya kutoa maamuzi juu ya miili yao.

2.6 Kusiwe na ndoa inayoendelea

Kifungu cha 15 kinaeleza kwamba kama mmoja wa wafunga ndoa ana ndoa ya mke mmoja basi hawezi kufunga ndoa nyingine.

Hali kadhalika mtu aliye na ndoa ya wake wengi hawezi kufunga ndoa ya mke mmoja. Pia kama mwanamke ana ndoa inayoendelea hawezi kuolewa tena na mwanaume mwingine.

2.7 Kusiwe na Pingamizi

Kwa mujibu wa kifungu cha 18 sheria inatamka kwamba kabla ya ndoa kufungwa ni lazima tangazo litolewe juu ya kusudio la kufunga ndoa. Kifungu cha 26 kinatamka kwamba tangazo hilo liwe la siku 21 kabla ya ndoa kufungwa. Hata hivyo, kifungu cha 23 kinaruhusu msajili wa ndoa kufungisha ndoa bila tangazo la siku 21 kama kuna sababu za msingi.

Lengo la tangazo ni kutoa nafasi kwa mtu mwenye sababu ya kuzuia ndoa hiyo isifungwe kuweka pingamizi dhidi ya ndoa hiyo kama inavyotakiwa katika kifungu cha 20(1). Kama pingamizi limewekwa, basi mfungishaji ndoa hawezi kuifungisha ndoa hiyo hadi pingamizi hilo litakapoondolewa.

Kifungu cha 20(2) kinampa nafasi mwanamke aliyeolewa katika ndoa ya wake wengi kupinga mume wake kufunga ndoa na mwanamke mwingine endapo huyo mke ana taarifa kwamba mwanamke anayetaka kuolewa na mume wake ana maradhi ya kuambukiza. Hata hivyo kwa kuwa UKIMWI ni ugonjwa ambao umeingia karibuni haijulikana kama pingamizi laweza kuwa mwanamke anayetaka kuolewa ana virusi vya UKIMWI.

2.8 Mfungishaji ndoa awe na mamlaka

Kwa mujibu wa kifungu cha 30(1) Sheria ya Ndoa, mfungishaji ndoa ni lazima apate leseni au kibali cha kufungisha ndoa kutoka kwa msajili mkuu wa ndoa.

2.9 Kuwe na mashahidi

Kifungu cha 27 kinaeleza kwamba ni lazima wakati wa kufunga ndoa kuwe na mashahidi wasiopungua wawili ambao ni lazima wawe na umri si chini ya miaka 18 na wawe na akili timamu na kuelewa lugha inayotumika. Pia ni lazima wawepo kwa pamoja kwenye tukio la kufunga ndoa.

2.10 Wafunga ndoa wote wawepo

Sheria katika kifungu cha 38(1)(f) inatamka kwamba wanandoa wote wawepo kwa pamoja wakati wa tukio la kufunga ndoa. Hata hivyo, kwa mujibu wa kifungu cha 38 (2) kama kuna sababu za msingi basi ndoa itafungwa bila mwanandoa mmoja kuwepo isipokuwa tu yule ambaye hayupo awe ametoa idhini hiyo mbele ya mshahidi.

Ni jambo la msingi kukumbuka kwamba kwa mujibu wa kifungu cha 38(1) shughuli zozote za kuwafungisha ndoa watu wasiokuwa na sifa za kuoana ni batili. Hivyo hata hiyo inayoitwa ndoa ambayo itakuwa imefungwa hali wahusika hawana sifa, si ndoa na ni batili tangu mwanzo wake.

3.0 AINA ZA NDOA

Kwa mujibu wa kifungu cha 9(2) na (3) kuna aina mbili tu za ndoa zinazotambulika, nazo ni ndoa ya mke mmoja na ndoa ya wake wengi.

3.1 Ndoa ya mke mmoja

Hii ni aina ya ndoa ambapo mwanaume anakuwa na mke mmoja tu.

3.2 Ndoa ya wake wengi

Aina hii ya ndoa inaruhusu mwanaume kuwa na mke zaidi ya mmoja. Kwa mfano, ndoa za kimila na za dini ya kiislam.

Kifungu cha 11 kinaruhusu wanandoa kubadili aina ya ndoa yao. Kama ilikuwa ya mke mmoja kuwa ya wake wengi au kama ilikuwa imekusudiwa kuwa ya wake wengi, kuwa ya mke mmoja. Hata hivyo kabla ndoa haijabadilishwa ni lazima kwanza wanandoa wakubaliane na watoe tamko kwa maandishi mbele ya jaji au hakimu juu ya uamuzi wao huo na wote watie saini zao.

4.0 UFUNGISHAJI NDOA

Kuna aina tatu za ufungishaji ndoa ambazo ni kidini, kiserikali na kimila kama ambavyo kifungu cha 25 (1) kinavyoeleza.

4.1 Ufungishaji Ndoa Kidini

Ndoa zinazofungishwa kidini hufuata taratibu za dini au madhehebu husika ambayo wanandoa ni waumini wa dini hiyo au madhehebu hayo.

4.2 Ufungishaji Ndoa Kiserikali

Sheria ya ndoa pia inaruhusu wanandoa kufunga ndoa kwa kufuata taratibu za kiserikali. Mara nyingi ndoa za kiserikali zinakuwa zikifungwa kwenye ofisi ya Mkuu wa Wilaya na zimekuwa zikifahamika maarufu kama “ndoa za bomani”

4.3 Ufungishaji Ndoa Kimila

Hizi ni ndoa zinazofungwa kwa kufuata taratibu za kabila husika ambalo wanandoa wanatoka.

Kila ndoa iliyofungwa aidha kidini, kiserikali au kimila inatakiwa isajiliwe kwenye daftari la Msajili Mkuu wa Ndoa kama inavyoelekezwa katika kifungu cha 43.

5.0 DHANA YA NDOA

Katika jamii zetu kuna aina ya mahusiano kati ya mwanaume na mwanamke wanaoishi pamoja na ambao hawakufuata taratibu za ufungishaji ndoa kama ilivyoelezwa hapo juu.

Sheria ya ndoa katika kifungu cha 160 inaeleza juu ya mahusiano haya kwamba endapo mwanamke akiishi na mwanaume kwa miaka miwili au zaidi mfululizo na jamii inayowazunguka ikawatambua na kuwapa hadhi ya mume na mke, basi mahusiano hayo yaweza kupata dhana ya kuchukuliwa kama wanandoa.

Ili kuwe na dhana ya ndoa pia ni lazima sifa za watu wanaotaka kufunga ndoa kama zilivyoenezwa hapo juu ziwe zimefuatwa. Kwa mfano, hakuna dhana ya ndoa endapo mmojawapo hajafikia umri wa kufunga ndoa.

Muhimu: Dhana ya ndoa ni dhana inayokanushika, yaani inaweza kupingwa mahakamani. Kukanusha au kuthibitisha dhana hii ni suala la ushahidi ambalo limewakosesha haki wanawake wengi. Hali yaweza kuwa mbaya zaidi pindi mmojawapo anapofariki kabla dhana ya ndoa haijathibitishwa.

Ni jukumu la watu wanaokaa katika mahusiano ya namna hii wafuate taratibu za kufunga ndoa mapema ili kuepuka matatizo ambayo yangeweza kuzuilika.

6.0 NDOA BATILIFU

Kwa mujibu wa kifungu cha 39 ndoa batilifu ni ndoa halali kisheria lakini kwa sababu fulani fulani mara tu baada ya kufunga ndoa inaonekana wafunga ndoa hao hawawezi kuendelea kwenye ndoa hiyo. Mambo yafuatayo yanaweza kuifanya ndoa kuwa batilifu:

- Kutoweza kufanya tendo la ndoa.
- Mmoja wa wanandoa kudhihirika kuwa na kichaa au kifafa.
- Mmoja wa wanandoa kudhihirika kuwa alikuwa ana magonjwa ya zinaa.
- Mke kudhihirika kuwa alikuwa na mimba ya mwanaume mwingine.
- Mwanandoa mmoja kukataa kwa makusudi kufanya tendo la ndoa tangu ndoa kufungwa.

Ndoa batilifu ni ndoa halali na itaendelea kuwa hivyo hadi hapo mahakama itakapoitengua.

7.0 HAKI ZA MWANAMKE KATIKA NDOA

7.1 Usawa

Sheria ya ndoa katika kifungu cha 56 inatamka bayana kwamba mwanamke aliyeolewa ana haki sawa katika kupata, kumiliki na kutumia mali yake kama ilivyo kwa mwanaume. Kwa ndoa za wake wengi, wanawake katika ndoa hizo wana haki sawa. Pia kifungu cha 66 kinakataza mwanandoa yeyote kumpiga mwenziwe kwa sababu yoyote ile.

7.2 Matunzo

Kifungu cha 63 kinatamka kwamba mume ana wajibu wa kumtunza mkewe kwa kumpa mahitaji yote muhimu katika maisha kama mavazi, chakula na malazi kulingana na uwezo wake. Mke pia atakuwa na wajibu huo ikiwa tu mume kwa sababu ya ugonjwa hawezi tena kufanya kazi yoyote. Na kama mume hatekelezi wajibu huo kwa makusudi mahakama chini ya kifungu cha 115 yaweza kumwamuru kutekeleza wajibu huo.

7.3 Kumiliki Mali

Mke ana haki ya kumiliki mali aliyoipata kabla ya ndoa. Ndoa haiwezi kuwa kigezo cha lazima cha kubadilisha umiliki wa mali ya mwanandoa isipokuwa tu kama wenyewe wamekubaliana hivyo na pia haimzuii mwanandoa kujipatia na kumiliki mali yake binafsi akiwa katika ndoa. Kifungu cha 58 kinaeleza haki hiyo.

7.4 Kuishi katika nyumba ya ndoa

Mke ana haki ya kuishi katika nyumba ya ndoa. Kifungu cha 59 kinaeleza kwamba nyumba ya ndoa ni ile ambayo wanandoa wanaishi. Hii inaweza kuwa nyumba waliyojenga au ya kupanga. Na kama nyumba ya ndoa ni ya kujengwa na wanandoa wenyewe, basi hakuna mwenye mamlaka ya kuiuza, kuipangisha au kuiweka rehani bila idhini ya mwanandoa mwenzake.

7.5 Kukopa

Mke ana haki ya kukopa kwa jina la mume wake au kuuza vitu vya mume kwa lengo la kujipatia mahitaji ya lazima ya familia.

7.6 Uhuru wa kuishi popote

Endapo mume atafariki kifungu cha 68 kinampa mjane haki ya kuamua akaishi wapi na asiolewe au aolewe na mtu ampendaye bila kuingiliwa na mtu au kufungwa na mila yoyote.

7.7 Kupata haki ya jasho lake

Mke ana haki ya kupata haki ya jasho lake alilochangia kwenye mali iliyopatikana wakati wa ndoa iwapo ndoa itavunjika kama inavyoelezwa katika kifungu cha 114.

8.0 KUTENGANA NA TALAKA

Kutengana na talaka ni haki alizonazo kila mwanandoa endapo ndoa yao itakuwa na matatizo kiasi kwamba itaonekana wazi kuwa wawili hawa hawawezi tena kuendelea kuishi pamoja.

8.1 Kutengana

Kutengana ni ile hali ya wanandoa kuacha kuishi pamoja, yaani kuacha kuishi chini ya dari moja

8.1.1 Aina kutengana

Kutengana kupo kwa aina mbili;

- i. Kwa hiari ya wanandoa wenyewe.
- ii. Kwa amri ya mahakama.

Amri ya kutengana kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 111 inawafanya wanandoa wasikae tu pamoja lakini haiondoi wajibu na majukumu aliyo nayo mwanandoa kuhusiana na matunzo.

8.2 Talaka

Talaka ni amri ya mahakama ya kuvunja ndoa. Chombo pekee chenye uwezo wa kuvunja ndoa ni mahakama tu. Mazoea ya wanandoa kupeana talaka mitaani aidha kwa maandishi au kwa mdomo, hizo si talaka kwa mujibu wa sheria ya ndoa. Ni lazima talaka itolewe na mahakama ili haki ya kila mwanandoa itamkwe bayana.


Kwa mujibu wa kifungu cha 100 mahakama haiwezi kusikiliza shauri la talaka kama ndoa haijadumu kwa miaka miwili. Ili shauri la talaka lipokelewe kabla ya miaka miwili ya ndoa kupita ni lazima mahakama itoe idhini. Idhini hiyo hutolewa pale tu ambapo mwanandoa mmoja anapata mateso yasiyokuwa ya kawaida.

8.2.1 Sababu ya kutoa talaka

Vifungu vya 99 na 107(1) vya sheria ya ndoa vinatamka kwamba sababu inayoweza kuifanya mahakama kutoa talaka ni pale tu itakaporidhika kuwa ndoa imevunjika kiasi ambacho haiwezi kurekebishika tena.

8.2.2 Sababu zinazofanya ndoa ionekane kuwa haiwezi kurekebishika tena ni:


- Ugoni na hasa kama tabia hiyo imeendelea hata baada ya mwanandoa mwingine kupinga tabia hiyo.



Epukana na uzinzi unahatarisha Ndoa yako na maisha yako

- Ukatili wa kiakili au wa kimwili ambao anatendewa mwanandoa mmoja au hata kama watoto ndio wanaofanyiwa ukatili huo.

- **Ulawiti**
- **Kuzembea wajibu** kwa makusudi
- **Utoro** au kutelekeza kwa makusudi kwa muda wa miaka isiyopungua mitatu.
- **Kifungo** cha maisha au kisichopungua miaka mitano.
- **Kutengana** kwa hiari au kwa amri ya mahakama kulikodumu kwa miaka mitatu au zaidi.
- **Kubadili dini.**
- **Kichaa kisichopona** ambapo madaktari bingwa wasiopungua wawili wamethibitisha kwamba hakuna matumaini ya huyo mtu kupona.
- **Kipigo**



Kupiga mke ni kosa la jinai “Hakuna mwenye haki ya kumpiga mwanandoa mwenzake”

8.2.3 Hatua za kufuata wakati wa kuomba talaka

Mtu yeyote anayetaka kuomba talaka mahakamani lazima kufuata taratibu zifuatazo;

- Kwanza kabisa kifungu cha 101 kinaeleza kwamba muomba talaka anatakiwa kupeleka malalamiko ya matatizo ya ndoa yake kwenye Baraza la Usuluhishi wa Ndoa la Kamishina wa Ustawi wa Jamii au baraza lingine linalotambuliwa kisheria kama kanisani au BAKWATA.
- Baraza la usuluhishi likishindwa kuwasuluhisha litatoa hati ya kwenda mahakamani. Hati hiyo huandikwa katika fomu maalumu inayoitwa “Fomu Na.3”. Kwa mujibu wa kifungu cha 106(2) madai ya talaka yanatakiwa kufikishwa mahakamani ndani ya miezi sita tangu tarehe baraza la usuluhishi la ndoa lilipotoa hati hiyo. Ni muhimu kufahamu kuwa baraza la usuluhishi la ndoa halina mamlaka ya kutoa talaka au kugawa mali za wanandoa bali kazi yake ni kusuluhisha tu.
- Baada ya hapo muomba talaka anatakiwa kutayarisha madai ya kuvunja ndoa na kuyawasilisha mahakamani akiambatanisha vielelezo vyovyote anavyoona vinaweza kuunga mkono madai yake. Kama shauri linafunguliwa mahakama ya mwanzo, basi mhusika anatakiwa kwenda kwenye hiyo mahakama na atapatiwa fomu maalum ambayo atajaza madai yake.

8.2.4 Mambo muhimu yanayotakiwa kuoneshwa kwenye madai;

- Kwamba kulikuwa na ndoa halali.
- Kuna mgogoro kati ya wanandoa hao na jitihada za kusuluhisha zimefanywa lakini imeshindikana.
- Orodha ya watoto wa ndoa na umri wao.
- Orodha ya mali za wanandoa hao walizochuma pamoja wakati wa ndoa yao.

8.2.5 Maombi kwa mahakama

Mwisho wa hati ya madai mwomba talaka anatakiwa aiombe mahakama itoe amri zifuatazo;

- Ndoa imevunjika kiasi isichoweza kurekebishika tena, hivyo talaka itolewe.
- Mgawanyo sawa wa mali zilizochumwa kwa pamoja kama inavyoelezwa katika kifungu cha 114. Pia kifungu hicho kinaeleza bayana kwamba mali iliyopatikana kabla ya ndoa lakini baadae ikaboreshwa kwa juhudi ya pamoja basi mali hiyo nayo huingizwa kwenye mali ya pamoja. Katika kulinda haki za wanawake, mahakama zimetoa tafsiri ya neno “juhudi ya pamoja” na kuhusisha kazi za nyumbani afanyazo mwanamke kama hakuajiriwa.
- Haki ya kuishi na watoto.
- Matunzo ya watoto kama bado ni wadogo.
- Gharama za kesi.
- Amri nyingine yoyote ambayo mahakama itaona inafaa.

Baadaye utatakiwa kuwasilisha madai hayo mahakamani na utapewa namba ya kesi na utaelezwa siku ya kesi.

8.2.6 Mahakama zenye Mamlaka ya Kusikiliza Madai ya Talaka

Mahakama zenye mamlaka kusikiliza mashauri ya ndoa ni Mahakama ya Mwanzo, Mahakama ya Wilaya, Mahakama ya Hakimu Mkazi na Mahakama Kuu. Mahakama hizi zote zina mamlaka sawa , yaani mtu anaweza kufungua shauri lake katika mojawapo ya mahakama hizo.

KARIBUNI WANAWAKE WOTE MPATE
USHAURI.

USIKUBALI KUONEWA,

USILALIE HAKI YAKO.

KITUO NI KWA AJILI YAKO WEWE.

Wasiliana nasi kwa anuani ifuatayo:

KITUO CHA MSAADA WA SHERIA KWA
WANAWAKE

MTAA WA KISUTU
JENGO LA WLAC,
KINONDONI HANANASIFU
S.L.P. 79212
DAR ES SALAAM